

# MAFANIKIO YA MRADI WA NISHATI SAFI NA SHIRIKISHI

Kutoka 2016 hadi 2020

Hivos
people unlimited



# MWANGA WA MATUMAINI: NISHATI JUDIDIFU YAPATA MSUKUMO TANZANIA

Licha ya Tanzania kuwa na vyanzo vingi vya nishati jadidifu, bado hajifanikiwa kutumia kikamilifu nishati hiyo salama na endelevu kwa ajili ya maendeleo.

Nchi hiyo ya Afrika Mashariki ni miongoni mwa nchi duniani ambazo zina rasilimali ya kutosha ya nishati jadidifu ikiwemo maji, jua, upepo, mawimbi, jotoardhi na biogesi.

Mpango Mkakati wa Uzalishaji wa Umeme wa mwaka 2016 (The Power System Master Plan 2016) uliotolewa na Wizara ya Nishati unaonyesha kuwa umeme unaozalishwa na vyanzo vya upepo, jua na jotoridi unachangia megawati 3.8 tu kwenye gridi ya Taifa yenye megawati zaidi ya 1,601.

Hadi kufikia Aprili 2020 kwa mujibu wa bajeti ya Wizara ya Nishati, zaidi ya nusu ya umeme huo wa gridi ya Taifa ulizalishwa na gesi asilia huku umeme wa maji ukichangia karibu asilimia 40 ya umeme wote.

Hata hivyo, safari ya Tanzania kuongeza matumizi ya nishati jadidifu imeanza kuleta matumaini baada ya Serikali kwa kushirikiana na wadau wa nishati kuanza mchakato wa kuandaa Mpango wa Taifa wa Nishati Jadidifu.

Kuundwa na kuanza kutekelezwa kwa mpango huo kutakua ni hatua muhimu kuongeza matumizi ya nishati jadidifu katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi nchini Tanzania.

Kwa sasa, Serikali ya Tanzania imepiga hatua katika uwekezaji wa nishati jadidifu ikilinganishwa na zamani lakini kasi hiyo itaongezeka zaidi ikiwa mchakato wa kuunda mpango huo utakamilika kwa wakati.

Waziri wa Nishati, Dk Medard Kalemani mapema Aprili 2020 alisema Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha wananchi na jamii ambazo hazijafikiwa na umeme wa gridi ya Taifa

zinaunganishwa na mifumo ya umeme jadidifu.
"Kazi zitakazofanyika mwaka 2020/21 ni pamoja na kuunganisha wateja na ufungaji wa mifumo ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na gridi zikiwemo taasisi za umma, visiwa katika bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Delta ya Rufiji," anasema Dk Kalemani katika bajeti ya wizara yake ya 2020/21.

Wadau wa nishati jadidifu wanapendekeza kuwa mipango kama hiyo italeta manufaa ikiwa Mpango wa Taifa wa Nishati Jadidifu utatekelezwa kwa kuhusisha wadau wote na kwa wakati.

## 'Yajayo yanafurahisha'

Hata wakati haijulikani bayana siku ambayo Tanzania itazindua Mpango wa Taifa wa Nishati Jadidifu, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia wameanza mchakato kuutengeneza mpango huo.

Jukwaa la Mabadiliko ya Tabianchi (Forum CC) ambalo ni mdau muhimu wa nishati kwa kushirikiana na wizara hiyo Juni 11 hadi 12, 2020 walifanya kikao maalum cha watalaam cha kukusanya maoni yatakayojumuishwa katika mpango huo.

Kikao hicho kilichofanyika jijini Dodoma, kilijumuisha watalaam kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais; Wizara ya Kilimo; Chuo Kikuu Cha Mzumbe; mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) na kampuni binafsi ambazo zinazijihusisha na shughuli za nishati jadidifu.

## Mchango wa Forum CC katika uanzishwaji wa mpango

"Forum CC tayari ilikusanya maoni ya kitaalam na kuwasilisha wizarani wakati tunasubiri kuanza kwa mchakato wa kuundwa kwa Mpango wa Taifa wa Nishati Jadidifu," anasema Mkurugenzi Mtendaji wa Forum CC, Rebecca Muna.

Kazi hiyo iliyofanywa na Forum CC ni sehemu ya mradi wa nishati safi na jumuishi (GEI) ambao taasisi hiyo ilikuwa inatekeleza kwa ushirikiano na shirika lisilokuwa la kiserikali la Hivos Afrika Mashariki kati ya mwaka 2016 na 2020.

Mradi huo ulikuwa na lengo la kuimarisha uwezo wa asasi za kiraia za kitaifa katika kuchagiza sera jumuishi zinazoshughulikia changamoto za mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na sekta ya nishati.

Pia mradi huo ulilenga kusaidia juhudi za kufikisha nishati kwa watu wote bila kujali hali zao kwenye jamii hususan maeneo ya vijijini na wanawake.

## Maeneo yatakayozingatiwa katika mpango huo

Kwa mujibu wa andiko la uchambuzi kuhusu msaada wa kitaalam kwa ajili ya Mpango wa Kitaifa wa Nishati Jadidifu uliotolewa na wizara hiyo na Forum CC, mpango huo utajikita katika maeneo makuu matano ya kimkakati ikiwemo ujumuishaji wa rasirimali zitakazotumika kutekeleza mpango huo.

Maeneo mengine ni kuhimiza matumizi ya nishati jadidifu, fursa za teknolojia zinazopatikana kwenye nishati na kuunda mifumo ya kitaasisi itakayofanya kazi kwa pamoja.

"Mpango utahakikisha unatambua athari chanya za usalama wa nishati na kufungua fursa za kukuza na kutangaza teknolojia za

nishati jadidifu," inaeleza sehemu ya andiko hilo.

Msingi na utambuzi wa maeneo hayo ya kimkakati umetokana na sera, mipango, changamoto na pengo la sasa lililopo katika sekta ya nishati jadidifu ili kuhakikisha inapewa msukumo wa aina yake wakati wa utekelezaji.

Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 inaitambua nishati jadidifu kama sekta muhimu inayoweza kuchangia maendeleo ya nishati nchini Tanzania kwa kurahisisha upatikanaji na matumizi yake.

## Nishati jadidifu inahitajika zaidi sasa kuliko mwanzo

Ikiwa mpango huo utakamilika na kuanza kutekelezwa utasaidia kuongeza kasi ya matumizi ya rasilimali za nishati jadidifu ili kukabiliana na changamoto za uzalishaji umeme hasa wa maji ambao umekuwa ukiathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Pia utekelezaji wa mpango huo utasaidia kuwapatia ahueni Watanzania ya gharama za nishati na kuwasaidia kupata nishati safi na salama ya kupikia na uendelezaji wa viwanda vidogo, jambo litakalowapatia fursa ya kupambana na umaskini wa kipato na kuboresha maisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Forum CC, Muna anasisitiza kuwa mpango huo unatakiwa upewe kipaumbele na uchukuliwe kama dharura kwa sababu ni kiungo muhimu cha upatikanaji wa nishati endelevu nchini Tanzania.

"Katika mpango huo mkakati utajumuisha njia zote za namna ya kutumia fursa za nishati jadidifu Tanzania na utasaidia katika tafiti, kupanga bajeti na kutoa miongozo kuhakikisha shughuli zote za nishati hiyo zinatekelezwa kikamilifu," anasema Muna.

Muna ambaye ni mdau muhimu wa mabadiliko ya tabianchi, anasema mpango huo utakuwa ni dira ya matumizi ya rasilimali zinazohitajika katika kuendeleza nishati jadidifu.

"Mpango utasaidia upatikanaji wa nishati safi na rafiki kwa mazingira ya kupikia na kukabiliana na ukataji wa miti, matumizi ya mkaa na changamoto za kiafya," anasema.

Mpango wa Taifa wa Nishati Jadidifu siyo tu utarahisisha upatikanaji wa nishati jadidifu lakini ni chombo muhimu cha utekezaji wa mpango wa Umoja wa Mataifa wa nishati endelevu kwa wote (SEAforALL) ambao Tanzania inautekeleza.

SEforALL inalenga kuwafikishia nishati watu wote, kuongeza ufanisi na ubora wa nishati mchanganyiko duniani.



# MKAA MBADALA UNAVYOBORESHA MAISHA YA WANAWAKE TANZANIA

Joto la saa saba mchana halikumzuia mama huyu kukoroga uji tayari akijiandaa kusonga ugali kwa ajili ya wateja wake watakaoanza kusogea mgahawani kwake ndani ya muda mfupi.

Hadi kufikia hatua ya kukoroga uji, mama huyo amemaliza kupika na kuunga nyama ya ng'ombe ambayo ilimchukua zaidi ya saa moja kuivisha.

Tofauti na mama lishe wengine, katika maandalizi ya chakula hicho, Amina Bakari (43) ametumia vipande vya mkaa visivyozidi 10 kukamilisha mapishi hayo.

"Unapika nyama, unaunga na unasonga hata ugali kwa mkaa huo huo unaouna jikoni," anasema Amina ambaye ananionyesha jiko lake la linalotumia mkaa mbadala.

Mama huyo ambaye huanza siku yake kwa kukaanga mihogo na kuwalisha chakula cha mchana wakazi na wageni wa mtaa wa Msimbazi ulipo karibu na soko la Tabata Muslim Jijini Dar es Salaam, ni mmoja kati ya wanawake 11 walioungana na kuunda kikundi cha Fahari Yetu ambacho kinajishughulisha na utengenezaji wa mkaa mbadala.

Kikundi hicho kilianza kutengeneza mkaa huo baada ya kupata mafunzo kutoka kwa jukwaa linalojihusisha na mabadiliko ya tabianchi la Forum CC chini ya udhamini wa Shirika lisilo la kiserikali la Hivos Afrika Mashariki (Hivos East Africa) mwaka 2018.

Mkaa huo unaotengenezwa na mabaki ya vyakula ikiwemo maganda ya ndizi na vifuu vya nazi ni mkaa wenye manufaa mengi siyo tu kupunguza gharama za kununua mkaa wa kawaida bali kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira.

"Mkaa wa kawaida ni mwepesi, ukiweka dakika moja umeisha hata maharage hayachemki. Lakini nikiweka huu, naweka maharage yangu yanaiva, nayaunga na watoto nawasongea ugali wanakula. Kwa hali yangu ya chini, mkaa

huu ni mzuri," anasema Amina ambaye ni mama wa watoto watatu.

Maganda ya mihogo anayopika Amina kwa sasa yana thamani hayatupi tena kwa sababu ni malighafi za kutengeneza mkaa mbadala ambao umechangia kuboresha maisha yake kutokana na biashara ya kuuza chakula.

"Zamani nilikuwa natumia Sh5,000 kwa siku kununua mkaa wa kawaida, siku hizi natumia Sh3,000, Sh2000 inayobaki naiweka naitumia kufanya mambo mengine," anasema Amina ambaye ni mmoja wa watengezaji wa mkaa huo.

Licha ya wanachama wa kikundi cha Fahari Yetu kutumia mkaa huo nyumbani na kwenye biashara za chakula, pia huuza kwa watu wengine hasa wamiliki wa migawaha wa Tabata.

"Mkaa huu umewanufaisha wengi kwa sababu tunatumia sisi na mwingine tunawauzia wenzetu wanaofanya biashara ya kuuza chakula," anasema Mwenyekiti wa kikundi hicho, Warda Sera (42).

Mkaa huo pia umesaidia kuboresha na kutunza mazingira ya soko la  Tabata Muslim kwa sababu mabaki ya vyakula na taka zingine zinatumika kama malighafi za kutengeneza mkaa mbadala.

## Jinsi mkaa huo unavyotengenezwa

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Warda Sera anasema matengenezo ya mkaa huo huanza na kukusanya taka za mabaki ya vyakula yakiwemo maganda ya ndizi, mihogo, matunda pamoja na vifuu vya nazi na kisha kuyakausha juani na baadaye kuchomwa moto kwenye mashine maalum.

Baada ya malighafi hizo kuchomwa, hutangwa kwenye vinu ili kupata unga wenye rangi nyeusi na kuchekeshwa kwenye nyujio ili kupata unga laini ambao huchanganywa na ujio wa muhogo au ngano ambao husaidia kugadisha malighafi hizo.

Malighafi hizo zote ambazo huwa katika hali ya uji uji huingizwa kwenye bomba maalum ambalo hukata vipande vya mkaa mbadala.
"Baada kukata vipande hivyo, tunaanika juani ili ukauke na tayari kwa matumizi. Zoezi la kutengeneza mkaa huu huchukua siku tatu kabla haujaanza kutumika," anasema Sera.

Kutokana na nguvukazi ya kikundi hicho, wana uwezo kuzalisha kilo 40 za mkaa mbadala kwa mwezi ambao hutumika katika shughuli zao na kuwauzia watu wanaowazunguka.

Licha ya kuwa mkaa huo una faida lukuki, akina mama hao wanaweza wakaongeza uzalishaji na kuwasambazia watu wengi kwa mkaa huo unaokoa mazingira, ikiwa watawezeshwa kupata teknolojia ya mashine za kisasa zinazorahisisha kazi ya uzalishaji.

Mwalimu wa mradi huo na Mkurugenzi wa taasisi ya Green Conservers ambao ni wataalamu wa kutenegenza mkaa mbadala, Baraka Machumu anasema kikundi hicho kinahitaji mashine zingine za kusagia na kuunda malighafi za mkaa mbadala ambao kwa sasa wanatumia mikono kutenengeneza.

"Hii mashine ya kuchomea malighafi inaambatana na mashine zingine mbili ambazo zote kwa pamoja zinauzwa kwa Sh2 milioni. endapo wakisaidiwa na kupata mashine zote, watakuwa hawana ulazima wa kutwanga wala kutengeneza maumbo ya mkaa kwa mikono," anasema Machumu.

Ikiwa kikundi hicho kitawezeshwa zaidi kifedha kitasaidia kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na ukataji wa miti Tanzania kwa ajili ya kuni na mkaa.

Mkurugenzi Mkuu wa Forum CC, Rebecca Muna anasema mradi huo wa mafunzo ya nishati safi ya mkaa mbadala ulihusisha makundi sita ya wanawake likiwemo la Fahari Yetu ambayo yalikuwa na watu 10 hadi 40 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam.

Makundi mengine yanayopatikana Ilala ni Buldoza, Watamgeta, Ushindi na Tupalane.
Muna anasema kuwa sababu za kuwahusisha wanawake katika mafunzo hayo ni kwa kuwa nishati za kupikia inamgusa mwanamke moja kwa moja kiafya, kiuchumi na kijamii.

Licha ya kuwa mafunzo hayo yalilenga wanawake wa Halmashauri ya Ilala, pia yaliwanufaisha watu mbalimbali wakiwemo wanaume kutoka mikoa ya Singida, Dar es Salaam na Dodoma.

“Wameongeza uelewa na ujuzi juu ya nishati jadidifu jinsi inaweza kuongeza kipato, jinsi inaweza kutunza mazingira na kuwasaidia katika shughuli zao za kila siku,” anasema Muna.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaaam, Godfrey Kizigo anasema kikundi cha Fahari Yetu kimekuwa mkombozi kwa mtaa wake kwani kimechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza uchafu wa mtaa huo.

“Wanakusanya taka, wanazichakata, hatimaye unapatikana mkaa. Umepunguza taka lakini pia umepunguza ukataji wa miti. Vyanzo vyetu vya miti vinapona,” anasema Kizigo ambaye kikundi hicho kinaendesha shughuli katika mtaa wake.



# MAJIKO BANIFU YANAVYOBORESHA MAISHA YA WANANCHI BAGAMOYO

Hapo nyuma wakazi wa viijiji vya Kidomole na Makurunge wilayani Bagamoyo, mashariki mwa Tanzania, walikuwa wakitumia fedha nyingi na muda kusaka nishati ya kupikia ambayo kwa kiwango kikubwa ilikuwa mkaa na kuni za miti ya asili.

Hata hivyo, huenda maisha yao yakachukua mwelekeo mpya baada ya kuanza kutumia majiko banifu yanayopunguza matumizi makubwa ya kuni na uharibifu wa mazingira.

Majiko hayo banifu ambayo hutengenezwa kwa malighafi za vyuma na mabati yanatumia kuni mbili kwa wakati mmoja kupikia, jambo linalowaondolea usumbufu watumiaji hasa wanawake kutumia muda mwingi kutafuta kuni porini.

Matumizi ya majiko hayo rafiki wa mazingira, yanatokana na mafunzo yaliyotolewa na asasi ya kiraia ya Mtandao wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ya CAN Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la kimataifa lisilo la kiserikali la Hivos Afrika Mashariki (Hivos East Africa) yaliyofanyika Julai 2020.

Mkazi wa Kijiji cha Kidomile, Mau Simba ambaye ni miongoni mwa watumiaji wa majiko hayo katika mgahawa wake, anasema amepunguza matumizi ya kuni ikilinganishwa na awali alipokuwa akitumia jiko la mafiga matatu.

Kwa kutumia jiko hilo, Maua anayefanya kazi hiyo kwa takriban miaka 20 sasa anaweza kupika chakula kingi kwa wakati mmoja kwa kutumia kuni chache, jambo lililomsaidia kupunguza gharama za kununua nishati hiyo.

“Kwa sasa natumia Sh2,000 kwa siku nne hadi tano kununua kuni ikilinganishwa na awali ambapo nilikuwa natumia hela hiyo kununua mzigo wa kuni kila siku,” anasema Maua ambaye sasa faida anayopata katika biashara imeongezeka kutokana na kupunguza gharama za kununua nishati.

"Sasa hivi kuna ahueni, watoto wangu wanafurahi kwa kuwa nawapa hela za kutosha wanapokwenda shuleni," anasema Maua.

Wakati Maua akipunguza gharama za kununua kuni, mwenzake Salma Tamla wa kijiji hicho, jiko hilo limeanza kuboresha afya ya familia yake hasa kumkinga na moshi ambao huathiri mfumo wa upumuaji na macho.

Majiko hayo ambayo yanadumu muda mrefu yanatoa moshi mchache, yanalinda na kuboresha afya ya familia; na wanawake kama Salma wanaweza kupata muda wa kukaa na familia na kufanya shughuli za ujasiriamali ili kujipatia kipato.

"Unaweza kupikia hata sebuleni na kuni zake na moshi usizagae kokote," anasema Salma.

Utengenezaji wa majiko hayo pia umesaidia kuondoa dhana iliyojengeka kwenye jamii kuwa wanawake hawawezi kufanya kazi zinazodhaniwa ni za wanaume ikiwemo kuchomelea vyuma.

Mariam Omary wa Kijiji cha Makurunge, aliyeshiriki mafunzo hayo ya kutengeneza majiko banifu, anasema kazi hiyo kwa sasa inampa furaha kwa sababu imeondoa uoga wa kufanya mambo yenye tija kwenye jamii bila kujali jinsia yake.

"Awali nilikuwa muoga kushika vitu vya umeme kiasi cha kushindwa kutengeneza majiko haya, kwa mtoto wa kike inataka moyo…namshukuru Mwenyezi Mungu nilipata ujasiri na sasa naweza kutengeneza ili kujipatia kipato na kutumia nyumbani, "anasema Mariam.

Majiko hayo banifu ikiwa yatatumiwa kikamilifu na Bagamoyo siyo tu yatasaidia kupunguza gharama za nishati ya kuni lakini ni njia rahisi kuelekea kutafuta suluhu ya kudumu ya ukataji wa miti na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania.

Ripoti ya Taifa ya Takwimu za Mazingira ya mwaka 2017 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kiwango cha ukataji miti kinakadiriwa kuwa ni hekta 372,000 kwa mwaka na kutishia uhai wa misitu iliyofunika hekta zaidi ya milioni 48 ya ardhi ya Tanzania.

Udhibiti wa ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa na kuni za majumbani na viwandani utasaidia kuendeleza mifumo ya maisha ya wanyama na mimea, kupunguza mmonyoko wa udongo na uzalishaji wa hewa ukaa na kutunza vyanzo vya maji.

## CAN Tanzania, Hivos walivyosaidia upatikanaji wa majiko hayo

Wakazi hao wa Bagamoyo wameanza kutumia majiko hayo nyumbani na kwenye shughuli za biashara baada ya kupata elimu kutoka kwa wenzao 10 ambao walipata mafunzo ya utengenezaji wa majiko banifu yaliyotolewa na CAN Tanzania.

Msimamizi wa miradi kutoka CAN Tanzania, Jophillene anasema waliamua kutoa mafunzo ya utengenezaji wa majiko hayo baada ya utafiti waliofanya kubaini kuwa asilimia 42 za kaya katika Wilaya ya Bagamoyo hazifahamu umuhimu wa nishati safi ya kupikia huku asilimia 91 ya kaya hizo zikitegemea mkaa na kuni kama nishati ya msingi ya kupikia.

Hii ni sawa na kusema kuwa kaya nne kati ya 10 wilayani Bagamoyo hazifahamu umuhimu wa nishati safi wakati kaya tisa kati ya 10 zikitegemea kuni na mkaa kupikia.

"Haya mafunzo ni miongoni mwa jitihada za kuhamasisha wananchi wa Bagamoyo kuachana na kuni na kugeukia mifumo ya nishati safi na rahisi ya kupikia," anasema Bejumula.

Anasema mafunzo ya nadharia na vitendo kuhusu utengenezaji wa majiko banifu kwa washiriki 10 wakiwemo wanawake wanne yamekuwa chachu kwa wakazi wa vijiji vya Kidomole na Makurunge kukabiliana na ukataji wa miti.

"Tulifanya mafunzo kwa siku tano na vijana walijifunza kutengeneza majiko mazuri ambayo yanapunguza matumizi kuni kwa karibu kwa asilimia 60," anasema Bejumula.

Mdau huyo wa masuala ya nishati jadidifu anaamini kuwa majiko hayo ni hatua ya awali ya kuwawezesha Watanzania kuachana na matumizi ya kuni na mkaa na kujielekeza katika nishati safi na salama ya kupikia ikiwemo gesi ya majumbani, umemejua na biogesi.

## Ni fursa ya ajira kwa vijana

Mafunzo ya utengenezaji wa majiko banifu yaliyotelewa na CAN Tanzania kwa kushirikiana na Hivos East Africa yanatakiwa kuungwa mkono na wadau mbalimbali wa mazingira ili kuwasaidia vijana kupata fursa ya kujiajiri na kujiongezea kipato.

Fundi wa majiko Ramadhan Rajabu (40) anasema utengenezaji wa majiko hayo ni rahisi, jambo linaloweza kuwasaidia vijana kuwauzia watu bidhaa hizo na kisha kuisaidia jamii inayowazunguka kutunza mazingira.

Anasema kwa siku anaweza kutengeneza majiko matatu na kila jiko huuzwa kwa wastani wa Sh30,000 hadi Sh35,000 kulingana na ukubwa wa jiko.

Baadhi wanaona elimu hiyo ni fursa ya kufungua viwanda vidogo vidogo vitakavyosaidia kutunza mazingira.

Swalehe Chingwa (23) anasema ana mpango wa kufungua kiwanda kidogo cha kutengeneza majiko banifu na wanahitaji usaidizi wa kifedha na mafunzo zaidi ili kuwafikia watu wengi na kuifanya dunia kuwa sehemu nzuri ya kuishi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kidomole wilayani Bagamoyo, Mrisho Some anahimiza wakazi wake zaidi ya 2,000 wa kijiji hicho ambacho kinakua kwa kasi kutumia majiko hayo ili kukabiliana na ukataji miti.

"Nitoe wito kwa wakazi wa Kidomole kuendelea kuchukua tahadhari za kimazingira ili kuhakikisha tunaendelea kukaa vizuri katika maeneo yetu na kutunza uoto wa asili katika kijiji cha Kidomole," anasisitiza Some.



# MAFUNZO YA NISHATI YALIVYOONGEZA CHACHU YA KURIPOTI HABARI ZA NISHATI JADIDIFU

Jennifer Gilla, mhariri wa lugha wa gazeti la Nipashe, hakuwahi kufikiria kuwa siku moja angeweza kusaka habari za nishati jadidifu na mazingira na kuchapisha kwa ubora kama wanahabari wengine.

Tangu ajiunge na tasnia ya habari, kazi yake ilikuwa ni kuhariri lugha katika gazeti hilo licha ya kuwa alikuwa akitamani kwenda kusaka habari zinazohusu mazingira.

“Mafunzo maalumu ya nishati jadidifu yalifungua milango lukuki ya kuiishi ndoto yangu ya kuwa moja ya wanahabari waliobobea wa nishati jadidifu,” anasema Jennifer ambaye amechapisha habari na makala lukuki za nishati jadidifu na mazingira.

Miongoni mwa makala zake mashuhuri iliangazia namna wanawake katika Kijiji cha Mpale wilayani Korogwe, Tanga wanavyotumia umemejua kukuza kipato kupitia biashara zao.

Jennifer alikuwa ni miongoni mwa wanahabari 20 wa mwanzo nchini Tanzania waliopatiwa mafunzo maalum ya namna ya kuripoti habari za nishati jadidifu kwa miezi sita yaliyoratibiwa na kampuni ya Nukta Afrika kwa ushirika na asasi ya kiraia ya kimataifa ya Hivos Afrika Mashariki.

Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Hivos Afrika Mashariki kupitia mradi wa kukuza matumizi ya nishati safi na jumuishi ujulikanao kwa Kiingereza kama ‘Green and Inclusive Energy’.

“Kwa sasa najiona kuwa nimebobea zaidi katika uandishi wa habari za nishati jadidifu na mabadiliko ya tabia nchi ambazo zinachangia kuboresha maisha ya watu wengi hususan vijijini,” Jennifer anasema.

Mafunzo hayo ya miezi sita yalilenga kuwawezesha wanahabri kuchunguza kwa kina matatizo yahusianayo na nishati, kuchambua na kuchapisha habari zenye

ushahidi wa kutosha na zinazochochea utatuzi wa changamoto mbalimbali.

Mafunzo hayo yalianzishwa ili kuongeza uelewa wa faida za matumizi ya nishati safi na kujenga mtandao wa wanahabari waliobobea katika kuripoti masuala ya nishati jadidifu.

Wanahabari waliohudhuria mafunzo hayo walifundishwa namna ya kutafuta habari za nishati jadidifu, kuchambua takwimu za sekta hiyo, kuandaa habari za kidijitali, kuandika habari zinazochochea suluhu katika jamii, masuala ya uhusiano wa nishati na jinsia na njia za kubaini na kukabiliana na habari za uzushi (Fact checking).

## Mafunzo yafungua fursa lukuki za kujifunza

"Tangu nihitimu mafunzo maalum ya kuripoti habari za nishati jadidifu nimekuwa nikipata fursa lukuki za kujifunza kuhusu nishati na mabadiliko ya tabia nchi ndani na nje ya nchi," anasema Jennifer, mhitimu wa Shahada ya lugha kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Jennifer alikuwa ni miongoni mwa wanahabari watatu ulimwenguni walioshinda fursa ya kwenda kushiriki na kuripoti mkutano wa kimataifa wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi jijini Bonn, Ujerumani mwaka 2019.

Kwa sasa Jennifer anaaminiwa na wahariri wake kuripoti habari za nishati jadidifu, jambo lililomshawishi kwenda kuchukua masomo ya juu ya uandishi wa habari.

Mafunzo hayo yamenufaisha wanahabari wengi hususan vijana kwa kuwaunganisha na vyanzo vya habari vikiwemo asasi za kiraia zinazohamasisha matumizi ya nishati jumuishi na safi.

Alfred Zacharia, aliyeshiriki awamu ya pili ya mafunzo hayo, anasema ushauri alioupata kutoka kwa wakufunzi mahiri na wazoefu umemwezesha kung'amua habari ya nishati jadidifu kwa haraka.

Maarifa hayo yamemsaidia kuchapisha habari kubwa ikiwemo iliyobaini namna tozo kubwa zinazotozwa na kampuni za gridi ndogo za umemejua zinavyopunguza kasi ya maendeleo vijijini.

"Nimebaini kuna fursa lukuki katika kuripoti habari za nishati jadidifu…wahariri na wamiliki wa vyombo vya wanapaswa kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika masuala haya," anaeleza Zacharia, mwanahabari wa gazeti la The Citizen.

## Habari za nishati jadidifu zaanza kung'ara

September 27, 2020 waandaaji wa tuzo mahiri za uandishi wa habari zinazotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) walimtangaza Sauli Gilliard kuwa mwandishi bora wa habari katika kundi la wazi mwaka 2019 baada ya habari iliyochunguza namna matumizi ya taa za barabarani za umemejua zilivyoongeza usalama na kipato kwa wafanyabiashara wanawake mkoani Lindi kushinda.

"Nawashukuru sana waandaji kwa kunipatia fursa ya kujifunza masuala ya nishati jadidifu na mazingira yaliyoniwezesha kushinda tuzo hii," anaeleza Gilliard ambaye ni mwanahabari wa gazeti la Daily News na Habari Leo. Habari ya Gilliard ni miongoni mamia ya habari zilizochapishwa kutokana na ruzuku ya kuripoti nishati jadidifu iliyotolewa na Hivos Afrika Mashariki.


Wadau wengine wa nishati jadidifu wanasema wamebaini ongezeko la habari kuhusu nishati jadidifu ndani ya mwaka mmoja uliopita kiasi

cha kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu nishati hiyo.

"Kuna habari nyingi sana na bora kuhusu nishati jadidifu...wanahabari ambao walikuwa kwenye mafunzo hayo wanaonekana kubobea, kujituma kwa ari kuhakikisha wanawaipatia jamii maudhui yenye ubora kwa ajili kuboresha maisha ya watu," anasema Sisty Basil, Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya kiraia ya Elico Foundation inayohamasisha masuala ya nishati jadidifu.

## Habari zaanza kuzaa matunda

Meneja Miradi wa Nukta Afrika, Maphosa Banduka anasema moja ya habari zilizochapishwa zilizifanya mamlaka kuchukua hatua ya kubadili jiko la msaada la kuokea mikate linalotumia umemejua baada ya kueleza kuwa liliharibika muda mfupi baada ya kufungwa wilayani Kisarawe katika mkoa wa Pwani.




Banduka anasema aina habari hizo ni moja ya malengo ya kuanzisha mafunzo hayo maalum kwa kuwa habari za nishati jadidifu hazikuwa kipaumbele kwenye vyombo vya habari miaka ya nyuma licha ya kuwa na mchango mkubwa kwa jamii.

"Tulitaka kubainisha mafanikio, na changamoto zinazoikabili sekta ya nishati jadidifu Tanzania ili fursa na hatua stahiki zichukuliwe na wahusika katika kukuza manufaa yatokanayo na nishati hiyo," anaeleza Banduka.

Banduka anasema wametoa mafunzo kwa wanahabari 40 kutoka maeneo mbalimbali Tanzania, idadi iliyosaidia kuunda mtandao wa wanahabari wa nishati jadidifu. Takriban wanahabari sita kati ya 10 ya waliopata mafunzo hayo walikuwa wanawake.

Awamu ya kwanza ya mafunzo ilifanyika kuanzia Desemba 2018 hadi Juni 2019 yakihusisha safari maalum ya kujifunza gridi ndogo za umeme vijijini, darasa maalum (Master Class), ruzuku ya kwenda kuripoti habari za nishati jadidifu na ushauri wa kitaaluma kutoka kwa wanahabari wabobevu kwa miezi sita.

Awamu ya pili ilianza Desemba 2019 hadi Julai 2020 ambapo Nukta Africa, Hivos Afrika Mashariki na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliongeza safari moja zaidi ya kwenda kujifunza miradi ya nishati jadidifu vijijini ili kujifunza zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET John Chikomo anasema kutokana na ujuzi walioupata na fursa kwa taasisi na wananchi wameamua kuweka rasmi masuala ya nishati jadidifu katika mpango mkakati wetu ujao wa mwaka 2021 – 2025 kwa kuwa awali walikuwa hawajihusishi sana na nishati jadidifu.

Hivos Afrika Mashariki inasema ushiriki wa vyombo vya habari katika kuongeza wigo wa kuelimisha umma kuhusu nishati jadidifu vijijini umeongeza maarifa kwa umma kuhusu uhusiano kati ya nishati na sekta nyingine kama afya na kuongeza uwazi katika masuala hayo.

"Vyombo vya habari vinaweza kuanzisha ajenda, kuwa mwangalizi wa sera za nishati jadidifu na kuwaonyesha watunga sera umuhimu wa masuala ya nishati jadidifu na mabadiliko ya tabianchi kwa wananchi," anasema Maimuna Kabatesi, Meneja Mradi wa Nishati Safi na Shirikishi (GIE).



# SAFARI YA MATUMAINI UJUMUISHAJI WANAWAKE SEKTA YA NISHATI TANZANIA

Katika jitihada za kufikia lengo la Nishati Endelevu kwa Wote (SEforALL), mapema Desemba 2018 Tanzania ilichapisha mpango wa utekelezaji wa jinsia maarufu kwa kimombo kama Gender Action Plan (GAP) unaolenga kuchochea usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wa wanawake kwenye sekta ya nishati.

Mpango huo unaotekeleza lengo la nishati endelevu kwa wote (SEforALL) ni kati ya hatua ambazo nchi hiyo ya Afrika Mashariki imezichukua baada ya kujiunga na Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 2012 baada ya ajenda hiyo kuhalalishwa duniani.

GAP, kwa mujibu wa Waziri wa Nishati, Dk Medard Kalemani, imelenga kutoa muongozo kwa wadau wote katika kuunda na kutekeleza malengo ya SEforALL huku ikichochea usawa wa jinsia na uwezeshwaji wa wanawake.

## Hatua moja kuelekea ujumuishi katika sekta ya nishati

Dk Kalemani anasema kabla ya GAP, Tanzania ilikuwa imeanzisha nyenzo za kufanikisha utekelezaji wa mpango nishati endelevu kwa wote zikiwemo Ajenda ya utekelezaji (Action Agenda) na Muongozo wa Uwekezaji (Investment Prospectus) tangu mwaka 2016.

“Kwa kuzingatia kuwa jinsia ni sehemu muhimu ya jitihada za SEforALL, GAP itatumika kama muongozo wa namna ya kuhusisha jinsia katika utekelezaji wa jitihada hizo ndani ya Tanzania kwa kutoa fursa sawa kwa wanaume na wanawake katika kufikiwa na kuongoza huduma za nishati endelevu kama haki ya msingi katika maendeleo,” Dk Kalemani anasema katika mpango huo wa GAP uliochapiswa mwishoni mwa mwaka 2018.

Tanzania ni miongoni mwa nchi duniani ambazo zimetekeleza miradi mikubwa ya nishati miaka ya nyuma lakini siyo miradi yote

ilikuwa na mitizamo ya kijinsia wakati wa hatua za upangaji na utekelezaji wake miongoni mwa taasisi za umma.

Kutengenezwa kwa Mpango wa Utekelezaji wa Jinsia ni matokeo ya mchango wa wadau wengi wakiwemo wa Serikali, kampuni binafsi na asasi za kiraia kama Mtandao wa Jinsia na Nishati Endelevu Tanzania (TANGSEN). TANGSEN ni Shirika lisilo la kiserikali linalochochea ujumuishi wa jinsia katika maendeleo endelevu ya nishati jadidifu.

TANGSEN ilifanya kazi kwa karibu na Wizara ya Nishati katika kuwajengea uwezo wa masuala ya ujumuishi wa jinsia viongozi wa serikali na taasisi pamoja na kutetea kuonekana kwa umuhimu wa jinsia katika sekta ya nishati.

"Mpango mkakati huu usingefanikiwa bila ya msaada wa kitaalamu wa masuala ya kijinsia kutoka kwa Mtandao wa Jinsia na Nishati Endelevu Tanzania, ambao walishirikiana na wizara ya nishati katika kufanya tathmini ya maandalizi ya awali ya mpango mkakati wa jinsia," Dk Hamisi Mwinyimvua, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anaeleza katika kitabu hicho cha SEforALL - GAP.

TANGSEN chini ya udhamini wa shirika lisilokuwa la kiserikali la Hivos Afrika Mashariki (Hivos East Africa) wamefanikiwa kuelimisha juu ya umuhimu wa kuchochea masuala ya jinsia ndani ya sekta ya nishati. Elimu hiyo imechangia katika kutengenezwa kwa mpango wa utekelezaji wa jinsia na baadaye kamati ya jinsia ndani ya wizara hiyo ya nishati.

Mchango wa TANGSEN kwa wizara ulikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa Hivos wa Nishati ya Safi na Jumuishi (Green and Inclusive Energy programme). Mpango huo una dhamira ya kufikia "mahitaji ya kinishati ya wanawake na wanaume katika shughuli zao za kila siku na kimaisha, hasa wanawake na kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabia nchi."

"Mpango wa utekelezaji wa jinsia wa mwaka 2018 unalenga kutatua masuala mbalimbali kama masuala ya nishati safi kwa ajili ya kupikia, nishati endelevu na masuala ya jinsia katika sekta ya nishati. Mpango huo ulitengenezwa kuisaidia Serikali kufanyia kazi masuala yanayohusisha jinsia," anasema Afisa Programu wa TANGSEN, Thabit Mikidadi.

Kwa mujibu wa Mikidadi, GAP imechangia kuundwa kwa kamati ya jinsia, chombo ndani ya wizara chenye malengo ya kuhakikisha wizara ina uwezo wa kutekeleza masuala ya kijinsia kwa vitendo.

"Kuundwa kwa kamati hii siyo shinikizo letu lakini ni matokeo ya kazi yetu. Baada ya kutoa elimu kwa wizara, wizara iliona umuhimu wa kuwa na kamati ya jinsia," anasema Mikidadi.
Malengo mengine ya mpango wa utekelezaji wa SEforALL-GAP ya mwaka 2018 ni kuchochea uwezo wa taasisi kuzingatia masuala ya kijinsia na kukuza uajiri wa wanawake na uwezeshwaji wa kiuchumi katika jitihada za SEforALL.

## Kwa nini jinsia ina umuhimu katika sekta ya nishati

Mikidadi anasema kuanzishwa kwa GAP kumesaidia kuyaweka masuala ya jinsia katika mwanga kuliko wakati mwingine wowote.

"Tulikuwa na vipindi vya kuwafundisha viongozi mbalimbali wa serikali za mitaa. Tuliwafikia maafisa wilaya na madiwani walioelimishwa kuhusu masuala ya nishati na jinsia," anaeleza Mikidadi.

Yapo mambo mengi ambayo serikali za mitaa na viongozi wa ngazi za chini wanaweza kuyafanya katika mipango ya nishati. Kwa kuwa sekta ya nishati haiwakilishwi katika ngazi za chini za serikali, mipango mingi huishia kutekelezwa kwa ngazi ya kitaifa kwa sababu wizara na mashirika ya kitaifa ndiyo yana uelewa mkubwa na mambo hayo, anaeleza.

"Unaweza kukuta mpango ni kujenga shule lakini usiwepo mpango juu ya umeme. Hivyo tuliwafundisha kufikiria nishati mbadala kama umemejua endapo wanaona hawajafikiwa na umeme wa gridi ya Taifa," anasema Mikidadi.

Elimu iliyotolewa pia ilizingatia nishati ya kupikia. Badala ya kuwaambia watu waache kutumia mkaa na kuni, nishati ambazo hutumika zaidi katika kupika nchini Tanzania, Mikidadi anashauri kuufundisha umma katika matumizi ya nishati endelevu kwa matumizi ya kupikia na teknolojia mpya zikiwemo majiko banifu yanayoendana na hali zao kiuchumi.

Nchini Tanzania, wanawake ndiyo huhusika zaidi katika kusimamia shughuli za kila siku za familia hususan katika maandalizi ya chakula hivyo hukumbana moja kwa moja na madhira ya njia zisizo rafiki za kupikia.

Kwa mujibu wa utafiti wa bajeti za kaya za mwaka 2017/18 (Household Budget Survey) uliotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kaya tisa kati ya 10 zinazoongozwa na wanawake Tanzania Bara (asilimia 91.6) zinatumia kuni na mkaa kama chanzo cha nishati ya kupikia ikiwa ni takriban kiwango sawa na zile zinazoongozwa na wanaume.

## Kufikiwa kwa watu wengi, safari yenye matumaini

Mikidadi anasema anafurahia kuona mashirika mengi, taasisi na hata Serikali zikitekeleza na kuthamini umuhimu wa kuzingatia masuala ya kijinsia hasa katika sekta ya nishati.

"Matarajio yetu makubwa kwa sasa ni kuzindua rasmi Mpango wa Utekelezaji wa Jinsia (GAP) kama kampeni ya kuongeza uelewa ili iwafikie watu na wadau wengine wa nishati. Hauwezi kujua nani mwingine atahitaji kushiriki katika kutekeleza kile kinachoshauriwa na mpango mkakati huo," anasema Mikidadi.



# ELIMU YA MKAA MBADALA INAVYOSAMBAA KWA KASI TANZANIA

Ni majira ya saa 5 asubuhi katika mtaa wa Mgeule, kata ya Buyuni katika Manispaa ya Ilala nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Hapo wamekusanyika wanawake na wanaume wapatao 10 katika chumba cha wazi kikiwa na vifaa mbalimbali yakiwemo maboksi, jiko, ndoo za maji, vinu na mfuko wa unga wa muhogo.

Watu hawa wanamsikiliza kwa makini mwezeshaji wa kike anayewafundisha kwa vitendo namna ya kutengeneza na kutumia mkaa mbadala unaotokana na taka.

Mkaa mbadala unaofundishwa hapa ni ule wa kutumia maboksi ya karatasi na chenga za mkaa wa kawaida, ikiwa ni moja ya hatua madhubuti za kudhibiti matumizi makubwa ya mkaa na kuni zitakanazo na miti ya msituni.

"Tumekuja hapa kutoa elimu ya mkaa huu ikiwa ni hatua ya kuwawezesha watu kufahamu fursa zilizopo kwenye mkaa mbadala," anasema Tausi Hassan, mkazi wa kata ya Kipunguni jijini Dar es Salaam ambaye anaongoza mafunzo hayo.

Uhodari na ujasiri wa Tausi (36) kutoa elimu ya mkaa mbadala ni matokeo ya mafunzo maalum ya utengenezaji wa mkaa mbadala aliyoyapata Oktoba 2019 kutoka kwa wataalam wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) chini ya ufadhili wa shirika lisilo kuwa la kiserikali la Hivos Afrika Mashariki (Hivos East Africa).

Mafunzo hayo ya jinsia na nishati yalilenga kuwajengea uwezo wa kutengeneza na kutumia mkaa mbadala wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala hasa wanawake ili kuwapunguzia gharama za kununua nishati ya kupikia na kuwalinda dhidi athari za kiafya ikiwemo magonjwa ya mfumo wa upumuaji na macho.

Mradi huo ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuhamasisha matumizi ya

nishati safi na jumuishi ulimwenguni wa Hivos ujulikanao kwa kimombo kama Green and Inclusive Energy.

Afisa Programu kutoka TGNP, Jackline Mwanyika anasema mafunzo hayo yalifanyika kwa awamu tatu ambapo watu 90 walifundishwa kwa nadharia na vitendo akiwemo Tausi anayeendelea kusambaza ujuzi huo kwa vikundi vingine kupitia kikundi cha cha Sauti ya Jamii.

Kikundi cha Sauti ya Jamii kutoka Kipunguni kilionyesha muitikio mzuri na kutaka kupata mafunzo zaidi ya utengenezaji wa mkaa huo na baadaye washiriki wake akiwemo Tausi wameendelea mpaka sasa kutoa elimu kwa watu mbalimbali jijini Dar es Salaam.

"Baada ya kupata mafunzo hayo, mara moja nikaanza kuyatendea kazi. Sasa ninatengeneza mkaa mbadala mwenyewe nyumbani ambao tunapika vyakula vingi kwa wakati mmoja," anasema Tausi ambaye pia ni mjasiriamali na mfugaji wa ng'ombe na kuku.

"Mkaa huu umenisaidia mimi na familia yangu, nilikuwa natumia mkaa wa zaidi ya Sh40,000 kwa mwezi lakini sasa ninatengeneza mwenyewe nimeshusha bajeti ya nishati kabisa," anasema Tausi.

Tausi anasema kwa siku anatengeneza kilo 25 za mkaa ambazo hutumia kwa siku tano hadi saba kwa matumizi ya kawaida ya familia yake yenye watu nane.

Licha ya kuwa mafunzo hayo yamempunguzia gharama za nyumbani, amekuwa balozi anayejitolea kusambaza maarifa na ujuzi wa kutengeneza mkaa huo kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam ili waachane na matumizi ya mkaa na kugeukia nishati safi ya kupikia.

"Watu wakielemishwa itasaidia wao kubadilisha mtazamo," anasema Tausi ambaye pia ni mwanachama wa kikundi cha maarifa na taarifa cha Sauti ya Jamii cha Kipunguni ambacho huwezeshwa na TGNP.

Mkaa huo mbadala ni rafiki kwa mazingira kwa sababu unapunguza ukataji wa miti, uzalishaji wa hewa ukaa na ni njia sahihi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine.

Ripoti ya hali ya upatikanaji na matumizi ya nishati ya mwaka 2016 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaeleza kuwa asilimia 88.2 ya kaya za jiji la Dar es Salaam zinatumia nishati ya mkaa kupikia huku zikitumia takriban asilimia 70 ya mkaa unaozalishwa Tanzania.

## Maarifa hayo yanayovyowafikia Watanzania

Mwenyekiti wa kikundi cha Sauti ya Jamii, Selemani Bishagazi anasema wanatoa mafunzo hayo kwenye vikundi mbalimbali vya kijamii na kiuchumi na mpaka sasa wamefundisha watu zaidi ya 550 jijini Dar es Salaam na mikoa ya jirani ikiwemo Pwani kuhusu utengenezaji wa mkaa huo.

"Tunataka watu waanze kwanza kutumia mkaa huu nyumbani ili jamii yote ikipata ujuzi ndiyo tuende kwenye hatua ya kutumia hata viwandani. Itasaidia sana kwa sababu mabadiliko yanaanza na watu wachache," anasema Bishagazi.

Siku zijazo, anasema, wanapenda kuona watengenezaji wa mkaa huo wanatumia teknolojia ya mashine za kisasa ili kutoa fursa ya kutengeneza mkaa mwingi utakaowaingizia kipato.

“Sisi tunasaidia jamii kupunguza gharama za maisha lakini kutengeneza biashara kwenye vikundi na kuona jinsi gani watu waliopata mafunzo haya, wanapata mitaji ya kununua mashine za kuzalisha mkaa mbadala,” anasema mdau huyo wa masuala ya jinsia na nishati.

Ili kupata mkaa mbadala wa wa maboksi, mtengezaji anahitaji maboksi yaliyokatwa vipande vidogo vidogo na kisha kulowekwa kwenye maji kwa saa 24 au kutwangwa kwenye kinu ili yalainike zaidi kabla ya kutengeneza kwenye maumbo madodo madogo kama mkaa.

Mkaa mbadala wa mabaki ya mkaa wa kawaida hutengenezwa kwa chenga za mkaa kuchanganywa na uji wa unga wa muhogo ambao hutumika kama gundi.

Baada ya hapo hukatwa katika maumbo madogo na kuanikwa juani kabla haujanza kutumika.

## Fursa zilizopo kwenye mkaa mbadala

Mkaa mbadala ni fursa ya kujiajiri kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vitakavyohusika na utengenezaji na usambazaji wa mkaa huo kwa watu ili kuongeza kasi ya kuhifadhi mazingira jijini Dar es Salaam.

Mwanzilishi wa taasisi ya Mabinti Safe Space Organization (Masaso) iliyopo kata ya Buyuni jijini Dar es Salaam, Aziat Juma ambaye amepata mafunzo hayo hivi karibuni anasema maarifa aliyoyapata kwenye mafunzo ya mkaa mbadala ni chachu ya kuanzisha kiwanda kwa sababu malighafi zinapatikana kirahisi.

“Ni wakati wa kuyafanyia kazi haya mafunzo, nitakaa na wenzangu…tuanze kutengeneza mkaa na kuuza kwa watu huku tukitoa elimu kuhusu faida zake,” anasema Aziat.

Anasema kiwanda hicho kitatoa fursa za ajira kwa wasichana ambao wamekuwa wakiwapigania kupata jukwaa salama la kutumia uwezo wao kujiletea maendeleo kwenye jamii.

Mwanyika anasema baada ya kutoa mafunzo hayo, hatua inayofuata ni kuangalia uwezo wa kuwawezesha watu walioonyesha muitiko mzuri kupata mitaji ili kuendeleza miradi ya utengenezaji mkaa huo katika maeneo yao.

“Tunatazamia kuwaunganisha na benki ili wapate mikopo itakayowezesha kununua mashine za kisasa ambazo zitarahisisha utengenezaji wa mkaa huo ili wapate kipato na kutunza mazingira,” anasema Mwanyika.

Kwa sasa, watengenezaji wa mkaa huo wanatumia mikono na zana duni, jambo linalowafanya wapate mkaa mbadala kwa matumizi ya nyumbani pekee na kuwakosesha fursa ya kufanya biashara inayotunza mazingira.

CAN
CLIMATE ACTION NETWORK
Tanzania

FORUM CC

NUKTA AFRICA
Lets grow together

tangsen
Mtandao wa Nishati na Jinsia Tanzania

TGNP

WAANDISHI MAZINGIRA

Hivos
people unlimited